Sustainable Development Verified Impact Standard

MRADI WA KASIGAU CORRIDOR REDD+ AWAMU YA KWANZA- ENEO LA RUKINGA.

Nakala hii imetayarishwa na Wildlife Works

WILDLIFE WORKS



Mpigaji picha: Filip C. Ago

Mradi wa Kasigau REDD+ Awamu ya I – Rukinga Sanctuary (KCRPI) iko Kusini Mashariki mwa Kenya katika Mkoa wa Pwani mwendo wa masaa mawili ukitumia gari kutoka mji wa bandari wa Mombasa. Eneo la mradi linaunganishwa na mazingira ya misitu iliyo kavu, inayotawaliwa na speshi kama vile akacia na komiphora na aina nyingine zinazostahimili ukame. Idadi kubwa ya watu katika eneo hilo wanatoka katika kabila la wataita, wengine wanao ishi katika maeneo hayo ni waduruma, wakamba na makabila mengine kutoka pande zote za nchi.

Eneo la mradi linahusisha eneo lote la ardhi ya Rukinga Sanctuari, na liko na jumla ya hekta 30,168.66 (eka74,516). Ardhi hiyo awali ilijulikana kama LR 12263, ambayo kihistoria ilikuwa imepunguzwa kwa ugavi 12263/1 na 12263/2 kabla ya tarehe ya kuanza kwa mradi.

Rukinga ni sehemu ya ardhi inayounda ukanda kati ya Hifadhi ya taifa ya Tsavo Mashariki na hifadhi ya Taifa ya Tsavo Magharibi. Ukanda huu unafika hadi safu ya mwisho ya milima ya Marungu. Eneo la mradi na eneo lisilo ndani ya mradi limeweka katika nyaraka Kielelezo 1, na mipaka yote zimepatikana katika vitabu za mkaguzi wa mradi. Ardhi iliyoko ndani ya mradi imeainishwa kuwa eneo lenyo misitu mikavu ya kitropiki kwa angalau miaka 20 na imekuwa misitu ambayo haijaguswa katika historia ya eneo hilo.

Lengo kuu la Shughuli za mradi ni kuanzisha miradi endelevu ili kuboresha maisha ya wananchi wa eneo hilo, hii imeweza kuafikiwa kupitia ajira ya moja kwa moja na pia kupitia miradi iliyoanzishwa ili kuzalisha mapato. Kwa wastani, Wildlife Works imeweza kutoa ajira kwa watu kati ya 50-53 kutoka katika eneo la mradi. Mbali na shughuli za msingi za mradi, mapato kutokana na mauzo ya hewa kaa kupitia Wildlife Works Carbon Trust (WWCT) yameweza kufaulisha miradi endelevu kwa jamii.

KCRPI hutoa faida nyingi ambazo zitasaidia Kenya kuafikia malengo ya maendeleo endelevu ya ulimwengu (SDGs). Mwaka 2015, Kenya ilijiunga na jumuiya ya kimataifa katika kupitisha malengo yake ya SDGs, ambayo ni seti ya malengo 17 ya ulimwengu wote yanayolenga kuangaza mazingira, uchumi na jamii. Mfumo huu umetengenezwa kusaidia kukusanya fedha na kuhakikisha kuna mipangilio ya kuboresha maisha ya wanadamu. Mwaka 2016, Kenya ilitekeleza mpango wa Dira ya maendeleo ya mwaka 2030, mpango wa maendeleo wa muda mrefu kwa lengo la kuigeuza Kenya kuwa nchi mpya ya viwanda na ya kipato cha kati ambayo inatoa maisha bora kwa raia wake wote ifikapo mwaka 2030. Hii yote itafanyika kupitia mfumo bora unao zingatia mazingira bora kwa wote.

Mipango hii miwili ya maendeleo endelevu inaratibiwa katika malengo yao na maeneo muhimu ya mradi. Mradi wa KCRPI unachangia nchi hii kuafikia malengo haya. Wildlife Works itatumia mfumo uliowekwa na kanunua za kufwatilia mradi wa CCB & SD VISta. SDGs ambazo KCRPI itachangia moja kwa moja katika ratiba zao.

- Lengo la kwanza: Kupunguza umaskini.
- Lengo la pili: Kuangamiza njaa.
- Lengo la tatu: Afya bora kwa wote.
- Lengo la nne: Elimu bora.
- Lengo la tano: Usawa wa Jinsia zote.
- Lengo la sita: Maji safi na salama kwa wote.
- Lengo la nane: Kazi na uchumi bora.
- Lengo la tisa: Miundombinu thabiti, Kuanzisha Viwanda na kuunga mkono Ubunifu.
- Lengo la kumi: Kupuguza ukosefu wa usawa.

- Lengo la kumi na mbili: Matumizi Endelevu na Mifumo ya uzalishaji.
- Lengo la kumi na tatu: hatua za kuangazia mazingira bora.
- Lengo la kumi na tano: Maisha mema duniani.
- Lengo la kumi na sita: Amani na umoja kwa maendeleo endelevu, Upatikanaji wa Haki kwa Wote, Ufanisi, Uwajibikaji, na Taasisi Jumuishi katika ngazi zote.
- Lengo la kumi na saba: Kuimarisha Njia za Utekelezaji na Kufufua Ushirikiano wa Kimataifa wa Maendeleo Endelevu.

Faida zinazotokana na mazingira bora ni kuhakikisha misitu iliyoko katika maeneo ya mradi imeweza kuhifadhi tani of 195,918 kwa ujumla za hewa chafu ya carbon wakati wa kipindi hiki cha ufuatiliaji na ukaguzi wa mradi Mradi huo utazalisha faida kubwa za jamii na viumbe hai. Fursa mpya za kuanzisha miradi endelevu zitawekwa, kama vile ajira ya moja kwa moja, shughuli mbadala za kuzalisha mapato (IGAs) na mipango ya kuchochea uwekezaji katika biashara zitaundwa ili kupunguza shinikizo kwa mazingira wakati wa kuongeza ustawi wa jamii. Miradi za ziada zitashughulikia usalama wa chakula, kuboresha vituo vya afya na elimu, pamoja na kuongeza elimu ya mazingira. Uhifadhi wa misitu na wanyama pori pia utachangia pakubwa kuhakikisha mradi unaendelea. Mradi huu pia unalinda makazi muhimu ya spishi nyingi zilizoorodheshwa na IUCN kuwa ziko hatarini kupotea, ikiwa ni tembo, zebra aina Grevi, Simba, Mbwa mwitu, chui, duma, Ndege aina ya Sekretari, ndege aina ya Martial Eagle, ndege aina ya Bateleur na aina kadhaa za volcha.

Faida kwa washika dau.

Faida ya kwanza	Wastani wa miaka mitatu iliyopita ya wafanyikazi 63 wa KCRP-Awamu ya I huku takriban 85% wakitoka eneo la karibu na 28% wanawake.
Aina ya faida	Hii ni faida nzuri na ambayo ni ya moja kwa moja.
Walio-faidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika	Ajira kuongezeka.

Faida ya pili	Mapato ya jamii/nyumba yaliyo juu ya (KES): <1,500 3% 1,500-5000 18% 5,000-10,000 40% 10,000-20,000 11% 20,000-50,000 4% >50,000 0%
Aina ya faida	Hii ni faida nzuri na ambayo ni ya moja kwa moja.

Waliofaidikia	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika	Uongezeko wa mapato kwa jamii.

Faida ya tatu.	99% ya kaya zinazozalisha mashambani kwa matumizi ya nyumbani na 29% ya kaya ziliuza mazao kwa pesa taslimu
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri na ambayo ni ya moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Ongezeko la mapato kwa jamii na pia kuweko kwa chakula ya kutosha.

Faida ya nne	Idadi ya wagonjwa ilikuwa ikiongezeka kwa kasi kabla ya kutatiza kwa COVID-19, kutokana na kuongezeka kwa rufaa katika Kaunti na kaunti jirani. Imekua kutoka kushughulikia wagonjwa wapatao 75 kwa mwezi tangu kufunguliwa Machi 2014 hadi karibu wagonjwa 250 kila mwezi kwa sasa, kila mmoja akifanyiwa vipimo kati ya 1-8 kulingana na utaratibu.
Aina ya faida	Hii ni faida nzuri na ambayo ni ya moja kwa moja.
Waliofaidika	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Kuboresha na upatikanaji rahisi kwa huduma bora za afya.

Faida ya tano.	Wagonjwa 3,000 waliopima 8,000 katika vituo vya afya vilivyoboreshwa
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Kuongezeka kwa fursa za elimu kwa vijana na wanajamii. Hii imeongeza wanajamii kuwa na fursa mingi kwa sababu ya elimu walionayo.

Faida ya sita	784 wanafunzi walikuwa wapokeaji wa bursary
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.

Ni nini ilyobadilika,	Ongezeko la fursa za elimu kwa vijana na wanajamii wenyeji, na hivyo kusababisha kuongezeka kwa uwezo wa watu binafsi katika jumuiya za mradi

Faida ya saba	Warsha 4 za mafunzo (pamoja na jumla ya wafanyakazi 65 waliohudhuria) zilizofanyika kwa ajili ya ujuzi/maendeleo binafsi.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini ilyobadilika,	Kuongezeka kwa fursa za elimu kwa wanajamii, na ambayo imesababisha kuongezeka wa kiwango cha uledi wa wanajamii kwa maswala ya miradi.

Faida ya nane	Miradi 5 ya ujenzi wa madarasa na ukarabati wa madarasa 3
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini ilyobadilika,	Kuongezeka kwa fursa za elimu kwa wanajamii, na ambayo imesababisha kuongezeka wa kiwango cha uledi wa wanajamii kwa maswala ya miradi.

Faida ya tisa.	Asilimia 25 ya walio katika nafasi za usimamizi ni wanawake
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Kuongezeka kwa fursa za ajira kwa wanawake katika mradi na kupunguza unyanyapaa katika nafasi zao za kazi.

Faida ya kumi	Watu 3,426 wanaopata vyanzo 10 vya maji vilivyojengwa na mradi
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Ongezeko la watu wengi kupata maji safi na salama kwa matumizi yao.

Faida ya kumi na moja.	<1% ngazi ya msingi; 2% ya sekondari; 1% ya wanafunzi wa elimu ya juu hawako shuleni kutokana na ukosefu wa ada.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Kuongezeka kwa upatikanaji wa elimu

Faida ya kumi na mbili	Asilimia 50 ya watu tuliohoji kutoka kwa idadi ya watu 185 katika mchakato wetu wa kuhoji wanajamii walisema kuwa maisha yameweza kuboreka na pia kipato kimeongezeka.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini imyobadilka.	Ongezeko ya elimu bora, ajira na huduma za kijamii.

Faida ya kumi na tatu	Asilimia 50 ya watu tuliowahoji walisema kuwa maisha yameboreka na wanawake wamechangia kwa kiasi kikubwa.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini ilyobadilika	Ongezeko la elimu bora, ajira na huduma za kijamii kwa wanawake.

Faida ya kumi na nne	Mikutano miwili ya hadhara na shughuli za kutoa elimu kuhusu REDD+.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo ni moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini ilyobadilika	Ongezeko la elimu kuhusu uhifadhi wa misitu na Wanyama pori na pia jinsi ya kuanzisha miradi endelevu ya jamii.

Faida ya kumi na tano.	Asilimia 66 ya wanajamii wanaelewa kuhusu uhiano ya misitu, mabadiliko tabia nchi and maswali ya miradi endelevu.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo inapatikana kwa eneo la mradi na ya moja kwa moja.

Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Ongezeko la elimu kuhusu mabadiliko ya anga, uhifadhi na njia za kuzuia na kuishi na mabadiliko yanayotokea.

Faida ya kumi na sita	3 taasisi za ndani kuundwa au kuimarishwa ili kuboresha ufanisi na uwajibikaji
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo inapatikana kwa eneo la mradi na ya moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Hukuza hisia dhabiti za kujitawala ndani ya jamii

Faida ya kumi na saba	8 mafunzo yanayohusiana na kilimo na kozi kwa matukio ya ugani
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo inapatikana kwa eneo la mradi na ya moja kwa moja.
Waliofaidika.	Wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Walioko saa hii na wa siku zijazo.
Ni nini iliyobadilika.	Kupitia mafunzo ya mbinu bora za kilimo kutakuwa na ongezeko la ufanisi wa matumizi ya rasilimali na kupitishwa zaidi kwa teknolojia safi na zinazozingatia mazingira katika kilimo katika jamii za eneo la mradi.

Faida ya kumi na nane	Mradi umeweza kuzalisha tani 195,918 za hewa kaa kutoka kwa uhifadhi wa misitu ukilinganisha na eneo lisilo kwa mradi ambalo pia tunatumia kulinganisha mabadiliko yanayotokea.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri ambayo inapatikana kwa eneo la mradi na kwa watu wote.
Waliofaidika.	Misitu yetu, bionuwai yote, viumbe ambavyo viko kwa kiwango cha kupotea kabisa, hewa safi inayosafishwa na misitu yetu kwa watu wote.
Ni nini iliyobadilika.	Mradi umechukua hatua kubwa wa kupunguza mabadiliko tabia nchi kutokana na uhifadhi wa misitu.

Faida ya kumi na tisa	Hectari 30,168.66 ya misitu imesimamiwa vizuri.

Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri na ya moja kwa moja.
Waliofaidikia.	Misitu yetu, bionuwai yote, viumbe ambavyo viko kwa kiwango cha kupotea kabisa, hewa safi inayosafishwa na misitu yetu kwa watu wote.
Ni nini iliyobadilika,	Kupitia ulinzi na uhifadhi wa misitu la eneo la mradi. Eneo hilo litakuwa na viwango vya ujasiri na uwezo wa kukabiliana na hatari zinazohusiana na mabadiliko tabia nchi na majanga yanayoweza kutokea,

Faida ya ishirini	Mitego 17 iliyopatikana; Mizoga 18 ya wanyama imerekodiwa.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri na ya moja kwa moja kwa watu wote.
Waliofaidika,	Bionuwai na Wanyama pori walio katika orodha ya kupotea.
Ni nini iliyobadilika.	Kupitia uhifadhi wa misitu na wanyama pori tumeweza kuzuia Wanyama pori walio katika orodha ya kupotea kutopotea.

Faida ya ishirini na moja	wawindaji haramu 7 na wachomaji makaa waliweza kutiwa mbaroni.
Aina ya faida	Hii ni faida nzuri. Inazingatia kulinda misitu na Wanyama pori.
Waliofaidika.	Bionuwai na Wanyama pori.
Ni nini iliyobadilika.	Upungufi wa uwindaji haramu na uchomaji wa makaa unao haribu misitu yetu katika eneo la mradi.

Faida ya ishirini na mbili	Aina tano za Wanyama pori walio katika hatari ya kupotea kulinga ya orodha ya IUCN wameonekana katika eneo la mradi.
Aina ya faida.	Hii ni faida nzuri na ya moja kwa moja kwa watu wote.
Waliofaidika,	Bionuwai na Wanyama pori walio katika orodha ya kupotea.
Ni nini iliyobadilika.	Kupitia uhifadhi wa misitu na wanyama pori tumeweza kuzuia Wanyama pori walio katika orodha ya kupotea kutopotea.

Wildlife Works imekuwa ikifanya kazi katika eneo la mradi kuanzia mwaka wa 1998 tofauti na mashikira mengine yasiyo ya kiserikali ambazo uanzisha miradi kisha kuondoka na kutembea mara kwa mara ili kuona jinsi yanavyoendelea, Kampuni hii imeweza kuajiri watu zaidi ya 100 katika shughuli mbalimbali ambazo zimeendelea na zimepanuliwa kutokana na fedha zinazopatikana kutoka kwa mradi wa Kasigau wa kulinda misitu na mazingira yake. Kampuni ya Wildlife Works imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo endelevu katika eneo la Rukinga tangu kuanza kwa mradi huo. Baadhi ya zile miradi iliyoanzisha ambayo inalenga kuinua maisha ya wakaazi na kulinda mazingira ni:

1. **Mradi wa kwanza ulikuwa ni ujenzi wa kiwanda cha kushona nguo** ambapo kiliajiri zaidi ya watu 150 wakati wa ujenzi kutoka kwa jamii iliyoko katika maeneo ya mradi. Wanawake kutoka eneo la mradi waliweza kufundishwa na kuajiriwa katika kiwanda hicho ili kushona nguo za pamba zilizozingatia uhifadhi wa mazingira. Nguo hizo ziliuzwa Marekani na bara la Ulaya na kuleta mapato kwa Wildlife Works and jamii ya eneo lini.

   Kiwanda hicho kimeonyesha ukuwaji mkubwa katika miaka ya hivi punde. Ingawa gojwa la uviko-kumi na tisa ilitatiza shughuli za kiwanda hicho, bado Wildlife Works kupitia washikadau wake wa kitaifa na kimataifa wameweza kuhakikisha shughuli zinaendelea kikamilifu. Kampuni hii inajivunia kuwa hakuna yeyote aliyepoteza ajiri katika kipindi cha uviko-kumi na tisa. Wildlife Works imeweza kudumisha uhusiano wake na kiwanda cha SOKO Kenya kilichoko mjini Mombasa ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa chuo cha kufunza jinsi ya kushona nguo kilichoko Mji wa Maungu..Mbali na ushonaji pekee, waonafanya kazi katika kiwanda hichi wameweza kupata mafunzo ya ziada inayowawezesha kufanya kazi popote. Mafunzo ya ziada waliopata ni kama vile kutafuta soko la mauzo, kuchapisha miundo kadhaa kwa nguo na mengineo.

   Kusaidia ushonaji, Wildlife Works imeweza kuanzisha kiwanda kingine kidogo kinachosadia kwa maswali ya uchapishaji (printing) ambapo kimeweza kuajiri zaidi ya watu tisa. Hiki kiwanda kimeweza kuzalisha bidhaa zinazotoka na ushonaji zinazouzwa katika soko la hapa nchini. Pia Wildlife Work wameweza kuweka maduka yanayouza bidhaa zinazotoka katika biashara hii ya ushonaji katika miji ya utalii kama vile Mombasa, Lamu na Nairobi. Kupitia maduka haya, soko limeweza kuongezeka na hii ni faida kwa Wildlife Works.

   Aidha, kiwanda kidogo cha sabuni cha Wildlife Works kilianzishwa na bado kinaendelea, kikiwa na wafanyikazi watatu walioajiriwa. Katika kiwanda hichi, sabuni tofauti tofauti hutengenezwa kutumia mafuta ya jojoba, maziwa ya nazi, mlimau na zinginezo. Sabuni hizi huuzwa katika masoko kadhaa yaliyoko miji mikuu kama vile Mombasa na Nairobi na pia kwa baadhi ya mahoteli za watalii nchini. Ingawa katika kipindi cha uviko kumi na tisa mauzo halitatizika katika soko la hapa nchini na kimataifa, shughuli za uzalishaji ziliendelea.

2. **Uuzaji na Soko za bidhaa**: Dhamira kuu ya Wildlife Works ni kutumia na kuweza kutafuta soko linalozingatia uhifadhi wa mazingira. Matumizi ya teknolojia bado ni sehemu muhimu ilikuendesha biashara zao Wildlife Works Inaendelea kujenga na kuboresha upatikanaji wa masoko ya bidhaa mbalimbali. Kupitia Kikundi cha wanajami cha Hadithi Crafts kinachoangazia kutafuta soko za bidhaa kadhaa kama vile vikapu vilivyosukwa kutoka kwa wanajamii. Kufikia Disemba 2020, wanajamii 8 waliweza kufunzwa jinsi ya kushona na wakapata ajira katika kiwanda cha Wildlife Works cha kushona nguo. Hadithi Crafts imeweza kutafuta soko kwa zaidi ya vikundi saba zinazotengeneza bidhaa kadhaa kutumia mikono, vikundi hivi saba viko na zaidi ya wanachama 226 wengi wao wakiwa wanawake. Katika kipindi cha uviko-kumi na tisa, biashara zilitatizika sana. Hadithi Crafts ilitafuta ufadhili mbadala wa misaada ya karibu dola 10,000 kusaidia vikundi hivi kabla ya biashara kurudi jinsi ilivyokuwa. Kupitia Hadithi Crafts, kiasi kikubwa cha mapato hurudishwa kwa wanachama iliwaweze kujikimu kimaisha. Mwaka 2017 Hadithi Crafts ilitumia shilingi 735,000 kununua bidhaa zilizotengenezwa na vikundi kadhaa, hizi pesa zililipwa moja kwa moja kwa watu binafsi ilikujiendeleza katika shughuli zao za kimaisha. Idadi hii iliongezeka hadi shilingi 1,575,000 mwaka wa 2018 na mwaka wa 2019 iliongezeka hadi shilingi 2,237,000. Fedha hizo zimeeendelea kuongezeka hadi kufikia shilingi 2,589,000 mwaka wa 2020. Katika kipindi cha kuripoti cha 2022, mauzo ya Hadithi chini ya KCRPI yalikuwa KES 2,489,255 (USD 20,043).Mbali na mauzo, Hadithi Crafts imeweza kutoka mafunzo mengi. Mwaka wa 2020,

vikundi saba vilipata mafunzo jinsi ya kusuka vikapu. Wanafunzi hao kwa sasa wanaweza kusuka vikapu kwa njia ya usadi na pia vikapu zao zimeweza kununuliwa na Hadithi.

3. **Mradi wa Kilimo endelevu:** Mradi huu uko na sehemu mbili. Ya kwanza kukuza miche na kuiuza na ya pili ni kilimo endelevu kupitia njia za kisasa. Wafanyikazi katika sekta hii wako na jukumu la kuhakikisha majukumu haya mawili yanafaulu. Kwa sasa sekta hii imekuwa na imeweza kutoa ajira kwa wanajamii zaidi ya 3 katika kipindi cha mwaka wa 2022. Uzalishaji na ukuzaji wa miche kama vile mitunda iliyo na citrus, maembe na parachichi na pia mboga imeweza kuboreshwa. Ufunguzi wa eneo la kuuza bidhaa zinazotokana na sekta hii kando kando mwa barabara kuu ya kutoka Mombasa kwenda Nairobi imeweza kuimarisha biashara. Ingawaje uviko-kumi na tisa ilisababisha biashara kwenda chini, kwa sasa imeanza kurudi jinsi ilivyokuwa.

   Wildlife Works inaendesha mradi wa upanzi wa miti na pia hununua miche kutoka kwa wakulima. Dhamira kuu ya huu mradi wa kukuza na kununua miche ni kuhakikisha tunakuwa na miti mingi katika maeneo ya jamii. Wildlife Works hununua miche na kuzirudisha bure katika maeneo ya jamii ambayo hayana miti. Hii imekuwa rahisi tukishirikiana na mashule pamoja na wanajamii.

   Kati ya miche za kiasili zilizo nununuliwa kutoka kwa jamii, kuna speshi tano ambazo zinafanya vizuri sana. Hizi ni: Vachellia robusta, Gardenia volkensii, Vachellia nilotica, Terminalia prunoides and Sclerocarya birrea. Pia miche za matunda kama vile pararachichi, mwembe na machungwa zinafanya vizuri sana katika eneo hili.

   Vikundi vine vya akina mama vinavyo jishughulisha na kilimo endelevu(Sechu, Kulikila, Lusario na Bungule) viliwezwa kusaidiwa kujikimu kibiashara na kupata ufadhili mbali mbali katika shughuli zao za kila siku.

4. **Kilimo katika maeneo makavu:** Wildlife Works inafanya kazi pamoja na shirika la utafiti wa maswala ya kilimo(KARI) ilikuangazia mimea inayoweza kustahimili ukame. Kwa sasa wanafanya utafiti wa mmea unaoitwa Jojoba unaokuwa katika maeneo makavu na unaweza kustahimili ukame, jojoba kupitia mbegu zake hutoa mafuta inayotumika kwa kazi mbali mbali. Lengo kuu ni kuhimiza uzalishaji wa mimea inayoweza kustahimili ukame ikizingatiwa eneo la mradi ni baadhi ya maeneo yaliyo na ukame.

5. **Kuboresha miundo misingi ya elimu na kupeana ufadhili wa karo kwa wanafunzi wanaotoka katika eneo la mradi:** Wildlife Works walipoanza kufanya katika eneo la mradi, viwango vya elimu vilikuwa chini sana. Kupitia mradi wa KCRPI wameweza kuboresha maeneo ya wanafunzi kusomea. Kwa sasa Wildlife Works wameweza kutengenezazaidi ya madarasa kumi na nane wakishirikiana na wanajamii wa eneo la mradi. Pia wameweza kutengeneza madawati na kupeana ufadhili kwa kulipia watoto karo.

6. **Utalii:** Mradi unaendelea kusaidia usimamizi wa Kambi ya Kivuli iliyoko Rukinga Sanctuary. Katika kipindi cha kuripoti 2022, jumla ya wageni 560 waliwekwa katika Kambi ya Kivuli, wakitumia jumla ya usiku 716 na usiku wa kulala 2294. Kambi ya Kivuli inaendelea kufanya kazi kikamilifu na inakaribisha wageni wa kigeni na wa ndani ikiwa ni pamoja na watalii na wageni wa elimu

7. **Ufatiliaje na ukaguzi wa mradi wa REDD+ unaofaulishwa na Wildlife Works.** Kila mwaka Wildlife Works hufanya ukaguzi wa mradi kuangalia kama yale waliokubaliana kufanya na kutekeleza yanafanywa kulingana na sheria zilizowekwa za mradi.. Wildlife Works huangalia kama misitu iko sawa na kama inaongezeka ama inapungua. Pia hutumia picha za satelite kuangalia uharibifu unaofanyika katika maeneo yaliyo ndani na nje ya mradi.

Mradi wa carbonulianza Rukinga lenye ukubwa wa ekari 74,490 kwa kuwa umiliki wa ardhi ulikuwa unauwazi na inatambulika kisheria.. Wildlife Works iliweza kuwapa mafunzo baadhi ya wafanyakazi ili kufanya hesabu ya miti, na kuajiri wataalam wa misitu kutoka eneo la mradi na nje ambao wako na uwezo wa kuelezea tofauti ya miti kama vile Commiphora na Acacia zilizopo. Takwimu zilionyesha kuwa Rukinga iko na miti zaidi ya milioni 6 na kanopi ya asilimia 30 ambayo kulingana na sheria za misutu inahitimu kuitwa msitu. Pia kikosi cha kukagua misitu na kuchukua takwimu kinazidi kuangalia maneno yaliyo nje ya mradi ambayo yanatumika kulingananisha.

8. **Maaskari pori wa Wildlife Works:** Rukinga Sanctuari ni shamba la kibinafsi kwa hivyo linakila haki ya kulindwa kutokana na watu kutoka nje. Wildlife Works imeweza kuajiri askari pori kutoka kwa maeneo ya wanajamii inayopakana na Rukinga na kazi yao kubwa ni kulinda misitu dhidi ya uvamizi haramu na uwindaji wa wanyama pori. Tuko na rekodi inayoangazia jinsi eneo hilo limeweza kulindwa kuanzia mwaka wa 1998 tulipoanza shughuli za uhifadhi. Mafanikio mengi ambayo Wildlife Works wameweza kupata ni kwa sababu ya ushirikiano walio nayo na wanajamii wanaoishi katika maeneo ya mradi. Pia Wildlife Works imeweza kutoa njia mbadala za kiuchumi kwa jamii ili kuweza kujikimu kimaisha na wasifikirie kuingia na kuharibu misitu na viumbe hai kaitka maeneo tunayofanya uhifadhi. Askari pori wa Wildlife Works hawana silaha na hii imeweza kuweka uhusiano bora na amani kati yao na wanajamii.

   Kikosi cha askari pori kimeweza kuongezeka hadi kufikia 25. Asilimia 10 ikiwa ni wanawake. Askari hawa hushika doria kila siku na wameweza kusambaa katika kambi 3 zilizoko katika eneo la mradi. Kambi hizi zimeweza kuwekwa katika mazingira bora na kuhakikisha ziko na maji safi na salama na pia umeme unaotumia makali ya jua. Ingawa askari pori wa Wildlife Works hawatumii silaha, wanashirikiana kwa karibu sana na maaskari wa KWS na uhusiano huu ulianza mwaka wa 2012 hadi leo. Kwa sasa KWS imeweza pia kuweka kambi kadhaa za maaskari ambazo ziko katika maeneo ya mradi.

   Hatimaye, Wildlife Works iko na ndege mbili aina ya gyrocopters ambazo ukusanya taarifa muhimu kutoka angani. Doria hizi za juu zimeweza kusaidia vikosi vya askari pori kufanya kazi kwa njia iliyobora an ya haraka na kuhakikisha misitu pamoja na viumbe hai wako salama. Pili, kupitia ndege hizi wameweza kupeana taarifa muhimu za maeneo la mradi. Robo ya visa vilivyo ripotiwa zilitokana na taarifa zinazotoka angani,

9. **Utafiti wa misitu, jamii na viumbe hai:**

   Wildlife Works iko na kitengo cha utafiti ambacho kiko na wafanyikazi wanne. Kazi yao kuu ni kufanya utafiti za kijamii na viumbe hai na pia kutathmini na kukusanya takwimu kutoka kwa vitengo mbalimbali. Kupitia hizi takwimu, tunaweza kujua kama tunaafikia malengo ya mradi na pia kuna athari gani zinazolenga mradi.

   Kambi ya utafiti ya Wildlife Works ilitengenezwa mwaka wa 2012 na kupanuliwa katika kipindi cha 2014-2016 ambapo eneo la watu haswa haswa watafiti wanaweza kuja na kupiga kambi huku na kufanya kazi zao. Mnamo 2022, nyumba tatu za ziada za wafanyikazi zilijengwa kuwaweka wanasayansi watafiti wakaazi.

10. **Walinzi:**

    Mradi wa miradi mingi ya usalama, hasa kuhusu ujangili ikiwa ni pamoja na kuongeza kikosi chetu cha mgambo hadi 25 (na takriban 10% wakiwa wanawake) ambao hufanya doria za kila siku za miguu na kuendesha doria kutoka vituo 3 vya nje vilivyosambazwa kote KCRPI. Vituo vyote vya nje vya mgambo vimetunzwa vyema Kikosi cha mgambo hakina silaha. Kwa sasa,

KWS ina timu kadhaa za kudumu zinazohamishika zilizoko kwenye ranchi kando ya Ukanda wa Kasigau (nyingi zikiwa ndani ya Mradi wa REDD+). Mradi bado unaendesha gyrocopter mbili ili kuwezesha tafiti za angani karibu kila siku kukusanya taarifa muhimu kwa madhumuni ya usalama na ufuatiliaji wa bioanuwai. Hii imesababisha ufuatiliaji bora wa spishi za Thamani ya Juu ya Uhifadhi pamoja na ugunduzi bora wa matukio; zaidi ya ¼ (25%) ya matukio yote yaliyorekodiwa katika kipindi cha kuripoti yaligunduliwa awali kutoka kwa doria ya angani.

11. **Kituo cha kutengeneza makaa zingira**: Wildlife Works ilianzisha kituo cha kutengenezea makaa zingira ambacho kiko katika eneo kubwa la uzalishaji karibu na mji wa MacKinnon Road katika eneo lililotengwa kwa ajili ya uzalishaji ndani ya shamba la Taita, Kwa sasa, kituo hicho kiko na wafanyi kazi 9 na wanaweza kutengeneza kati ya 1000 hadi 1500 ya makaa zingira kila wiki. Mpango huu wa biashara ya kutengeneza makaa zingira uliungwa mkono zaidi na Mfuko wa Taifa wa Utafiti wa Kenya (KNRF) na wakaweza kununua mashine za kutengeneza makaa zingira za kisasa na pia kuwasaidia kwa maswala ya kutafuta soko. Katika kipindi cha kuripoti cha 2022, mashine ya kukamua briquette, mashine ya kusagia na mchanganyiko zilipatikana kwa ajili ya kutengeneza briketi ndogo zenye umbo la mto, pamoja na tanuru iliyoboreshwa ambayo ilibuniwa na kujaribiwa kwenye tovuti. Uchambuzi kamili wa mchakato wa uzalishaji utawezesha kuongeza hadi hali ya nusu ya kibiashara.
12. **Msaada unaotolewa na Wildlife Works ilikuhakikisha usajili wa Tsavo Conservancy unafanyika:** Mchakato wa kusajili Tsavo Conservancy ulikuwa unaenda polepole sana kuanzia mwaka wa 2018 hadi 2019. Hii ilisababishwa na kuweko na ugumu wa kisheria na mfumo mpya wa ugatuzi uliokuja. Kenya Wildlife Conservancy Association, KWS na serikali ya kaunti zinaendelea kuhakiksha kwamba mchakato huo unaendelea na kumalizika wakati unaofaa. Wildlife Works inaendelea kutoa msaada kwa kuhakikisha vigezo vyote vinahitajika ili kusajili Tsavo Conservancy vinapatikana. Kupitia uwekezaji kama vile kuundwa na kuboreshwa kwa hoteli ya Kivuli na Satao Camps inachangia mchakato huu wa usajili kwani inaonyesha kuwa ni muhimu na yanafaa kuwekwa katika ngazi ya conservancy. Wildlife Works inaimani kuwa mchakato huu utaisha karibuni na maeneo haya kupewa hadhi ya kuitwa conservancy. Wildlife Works pia inapambana kuhakikisha pia eneo la Wanyama pori la Rukinga linapata hadhi hiyo hiyo.
13. **Miradi za kiafya za Wildlife Works**: Wildlife Works imejitolea kusaidia miradi za jamii. Wildlife Works inaamini kwamba ili jamii kuendelea lazima waweke elimu ya jamii kipa umbele. Moja ya malengo ya Wildlife Works ni elimu, hasa kwa wanawake na wasichana, lakini pia kwa wanafunzi wa kiume. Ingawa gonjwa la uviko-kumi na tisa ulivuruga mpangilia wa elimu na kusababisha shule nyingi kufungwa, Wildlife Works waliweza kutoka elimu ya afya unaolenga wasichana wanaotoka katika familia zinazoishi katika mazingira magumu ya kifedha na Maisha. Pia waliweza kuwa na vikao 2 vilivyohusu elimu na mafunzo mafunzo ya afya ngono na usafi kwa wasichana. zaidi ya wasichana 273 kutoka maeneo ya mradi waliweza kupata mafunzo haya. Pia Wildlife Works waliweza kusambaza sodo 121 zinazoweza kutumika zaidi ya mara moja kwa wasichana wanaishi katika maeneo ya mradi.
14. **Maskauti wanao saidia na uhifadhi wanaotoka katika maeneo ya jamii**: Wildlife Works inashirikiana na wanajamii katika maeneo matatu ya mradi zikiwa ni: Makwasinyi; Sasenyi; and Kale/Buguta/Mkamenyi/Birikani.Katika maeneo haya, wanajamii waliochaguliwa na wako na tajriba ya maswala ya uhifadhi uchukua takwimu ya wanyama wanaoingia vijijini na kupeana taarifa muhimu za jinsi jamii wanaishi na wanyama pori. Hii imeweza kusaidia na kuhakikisha

maeneo yaliyoko na mkwaruzano mkubwa kati ya wanyama pori na binadamu yanangaziwa na njia mbadala za kuzuia mikwaruzo zaidi zinawekwa.